

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA THELATHINI NA MBILI

19 JUNI, 2015



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA THELATHINI NA MBILI – TAREHE 19 JUNI, 2015

I. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

224. MHESHIMIWA DEO KASENYENDA SANGA (NJOMBE KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-
Tuliomba barabara ya kutoka Mtwango kupitia Kichiwa hadi Ikuna, Nyombo; pia barabara ya kutoka Makambako – Mlowa – Manga – Usetuke – Kifumbe – Ibatu – Kitandililo kuunganishwa na barabara ya Mgololo:-

(a) Je, ni lini barabara hizo zitapandishwa hadhi na kuwa za Mkoa;

(b) Je, ni lini zitaanza kutengenezwa.

**225. MHESHIMIWA HAMOUD ABUU JUMAA
(KIBAHA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Ombi la Barabara ya Vigwaza kupewa hadhi ya kuwa barabara ya Mkoa ni la muda mrefu sana; lakini hadi sasa ombi hilo bado halijapatiwa ufumbuzi:-

Je, ni lini barabara hii itapandishwa hadhi na kuwa barabara ya Mkoa.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**226. MHESHIMIWA CONCHESTA LEONCE
RWAMLAZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Nyumba za Askari Polisi na Magereza zilizopo kwenye eneo la Nshambya na Miembeni katika Manispaa ya Bukoba ni za miaka mingi na zimechakaa sana:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia Askari hao makazi bora.

227. MHESHIMIWA VICENT JOSEPHAT NYERERE (MUSOMA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Uchumi wa nchi unakua kwa asilimia saba (7) kwa mwaka lakini hakuna uwiano mzuri wa kimataifa kati ya polisi na raia, na vijana wengi wapo tayari kujiunga na Jeshi la Polisi.

Je ni lini Jeshi la Polisi litaajiri japo vijana 30,000 kwa mwaka.

228. MHESHIMIWA MUHAMMAD IBRAHIM SANYA (MJI MKONGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Wawekezaji wengi wameonyesha dhamira ya kuwekeza katika Sekta ya Kilimo na Viwanda hapa nchini; na wengi wa hao wawekezaji tayari wako nchini wanaendelea na shughuli zao lakini baadhi ya Wananchi wamekuwa wakichoma moto nyumba zao na mali zao:-

Je, Serikali inawachukulia hatua gani Wananchi wanaofanya uhalifu huo.

WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

229. MHESHIMIWA LOLESIA JEREMIAH BUKWIMBA (BUSANDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-
Mhe. Rais katika mkutano wa hadhara
mwaka 2010 aliwaahidi wachimbaji wadogo
wa Kijiji cha Nyarugusu kuwa watatengewa
maeneo ya uchimbaji:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo.

WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

230. MHESHIMIWA MOSHI SELEMAN KAKOSO (MPANDA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo,
Chakula na Ushirika:- Zao la Tumbaku
limeshuka bei kwenye soko la dunia, wakati
wakulima wa zao hilo wakiwa wamezalisha
tumbaku kwa wingi kupitia hamasa
iliyotolewa na Waziri Mkuu Mstaafu, Mhe.
Edward Lowassa na Waziri Mkuu wa sasa
Mhe. Mizengo Pinda:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwafidia
hasara waliyoipata wakulima wa zao hilo
nchini.

WIZARA YA MAJI:

231. MHESHIMIWA MARIA IBESHI HEWA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Wananchi wataruhusiwa kunywa maji ya bomba moja kwa moja bila ya kuchemsha.

232. MHESHIMIWA PROF. DAVID HOMELI MWAKYUSA (RUNGWE MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-
Mradi wa Maji wa Masoko Wilayani Rungwe uliotarajiwa kunufaisha Wananchi wa vijiji 15 ulisainiwa mwaka 2009 na ulitegemewa kukamilika na kukabidhiwa kwa Wananchi mwezi Agosti, 2011 lakini hadi leo hakuna hata Kaya moja iliyopatiwa maji ya mradi huo:-

Je, Serikali ina nia ya kweli ya kuwapatia Wananchi hao maji hasa ikizingatiwa kuwa miradi mingi mipya imeanzishwa humuhumu nchini na kukamilika wakati mradi wa Masoko ambao ungekamilika miaka minne (4) iliyopita bado unawekwa kando.

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

233. MHESHIMIWA SALUM KHALFANI BARWANY (LINDI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi:- Serikali imejenga Chuo cha **VETA** Lindi na pia ilikuwa na mpango wa kujenga hoteli kwa lengo la kutoa mafunzo kwa vijana wetu:-

- (a) Je, Serikali imefikia wapi kwa suala la ujenzi wa hoteli hiyo;
- (b) Je, **VETA** wana mpango gani wa kuwa na kiwanda cha minofu ya Samaki kama kile cha Dodoma.

II. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)

Kwamba, Bunge likubali kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2014 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

WAZIRI WA FEDHA:

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha, 2015/2016.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
19 JUNI, 2015**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**

